# VIPENGELE VYA KIONTOLOJIA VINAVYOUNDA JAALA ZA MASHUJAA KATIKA TENDI ZA NANGA

***Hellen Lyamuya***
*Chuo Kikuu Kikuu cha Dar es Salaam - Tanzania*
Hellen_lyamuya@yahoo.com

## Ikisiri

*Makala hii inachunguza vipengele vya kiontolojia vinavyounda jaala za mashujaa katika tendi za Nanga. Wataalamu waliotangulia hawajatilia mkazo nafasi ya ontolojia ya Kifrika katika kuunda jaala za mashujaa wa tendi za Kiafrika. Lengo la makala hii ni kuweka bayana vipengele vinavyounda jaala za mashujaa katika tendi za Rukiza na Mugasha. Makala hii imetumia utafiti wa maktabani na uwandani. Mbinu zilizotumika ni mbinu ya uchanganuzi wa matini na mahojiano. Sampuli ya utafiti ni wapiga Nanga, wazee na vijana wanaopatikana Mkoa wa Kagera. Matokeo ya uchunguzi uliofanywa yameonesha kuwa jaala za mashujaa wa tendi za Nanga zinaundwa na vipengele vya ontolojia ya Kiafrika kama vile kuthamini uzazi, kuheshimu wahenga, uanthropomofia, nguvu ya kani, umoja na mshikamano na uhusiano wa maumbile na vilivyomo.*

## 1.0 Utangulizi

Tendi za Nanga ni ushairi wa kiutamaduni ambao unapatikana katika eneo la ukanda wa maziwa makuu, yaani Uganda, Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Jina la 'Nanga' linatokana na ala ya muziki yenye umbo la mtumbwi na nyuzi saba inayopigwa wakati wa kuimba ushairi huu. Muktadha wa kihistoria unaonesha kuwa tendi hizo zinafungamana na utamaduni wa Wahaya wanaopatikana katika jamii za Tanzania (Mulokozi, 2002). Suala hili linadhihirisha kuwa tendi hizo zinafungamana na ontolojia ya jamii za Kiafrika. Mbiti (1969), Mbijima (2016) na Mulokozi (2017) wanaeleza kuwa ontolojia ya Kiafrika inafungamana na maarifa, mtazamo na imani ya Waafrika kuhusu maisha,

kuwapo kwa mwanadamu na ulimwengu kwa ujumla. Katika tendi za Kiafrika imani na mitazamo hiyo inajidhihirisha kupitia jaala za mashujaa.
Msingi mkubwa wa jaala umekitwa katika imani ya kutokuepukika kwa matukio yanayompata mwanadamu licha ya jitihada za binadamu kuyakwepa. Matukio yanayompata binadamu hutokana na mpango na utaratibu ambao mwanadamu hawezi kuuzuia. Mtazamo huo katika ontolojia ya jamii za Kiafrika unafungamana imani kwamba mwanadamu hawezi kubadilisha mkondo wa maisha yake ambao umepangwa na Muumba wake (Wamitila, 2003; Ponera, 2014; Charles, 2019). Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kuna nguvu za kiontolojia zinazomwezesha mwanadamu kutimiza jaala yake au kudra (mipango iliyopangwa na Mungu juu ya maisha yake).

Kwa upande wa kazi za fasihi, Vázques (1973), Mulokozi (2002; 2017), Finnegan (2012), na Mnenuka (2020) wanadai kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya sanaa na jamii. Wasanii kama sehemu ya jamii huunda sanaa kulingana na uhusiano wao na jamii. Hii ina maana kuwa sanaa na jamii zimefungamana. Hakuna shaka kwamba kazi za fasihi haziibuki katika ombwe bali zinachimbuka kutokana na mifumo anuwai ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii (Innes, 1974; Mutembei, 2000; Samwel, 2015; Mulokozi, 2017). Kiutamaduni, jamii zinafungamana na ontolojia ya jamii inayojumuisha mfumo mzima wa maisha ya jamii, mila, desturi na imani zinazoongoza maisha ya Waafrika (Mbiti, 1969; Makumba, 2005). Kutokana na muktadha huo, ni dhahiri kwamba kazi za fasihi zina uhusiano na ontolojia ya jamii. Kwa upande wa ushairi simulizi hususani tendi simulizi, ontolojia inayojitokeza katika kazi hizo imechukua sura tofauti. Msisitizo mkubwa katika uchambuzi wa masuala ya kiontolojia yanayofungamana na jaala za mashujaa umeegemezwa katika ontolojia za Kimagharibi. Aidha, ontolojia ya Kiafrika inayojitokeza katika tendi imedunishwa na kuonekana kuwa ni mambo yanayofungamana na ujumi wa mwandishi au yeli na hayana umuhimu wowote katika jaala za mashujaa wa tendi za Kiafrika (Bowra, 1964). Kwa kutambua hilo makala hii imefafanua jinsi vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vinavyounda jaala ya shujaa katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha*.

## 2.0 Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Mwasisi wa nadharia hii ni Placide Tempels katika kitabu chake kinachojulikana kama *Bantu Philosophy* (1945). Tempels anaeleza kwamba kwa Wabantu, Ontolojia ya Kiafrika inafungamana na kani uhai. Kani uhai inahusishwa na Mungu, uungu, mwanadamu na jamii. Kani hizi zinaweza kudhoofisha au kuimarisha maisha ya binadamu. Baadhi ya Waafrika walioendeleza nadharia hii ni pamoja na Kagame (1956), Mbiti (1969), Kezilahabi (1985), Makumba (2005), Mihanjo (2004) na Mulokozi (2017). Wataalamu hawa wanaeleza kwamba Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inajumuisha misingi kama vile dini, uanthropomofia, familia pana, ulimwengu wenye nyuga tatu,[23] kuheshimu wahenga au mahoka, kuthamini sana uzazi, miungu wengi, mapepo, imani katika sihiri na uchawi, uyakinifu wa kipragmantiki,[24] na dhana ya wakati. Misingi mingine ya Ontolojia ya Kiafrika ni ujamiishaji wa kiduara,[25] kuthamini kazi, itikadi ya kani, mtazamo wa umosi, matambiko, nguvu hai, familia pana, umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo na jaala badilifu.

Makala hii imetumia baadhi ya misingi inayofungamana na ontolojia ya Kibantu kuchambua vipengele vya kiontolojia vinavyounda jaala za mashujaa katika tendi teule. Miongoni mwa misingi hiyo ni kuthamini sana uzazi. Katika jamii za Kiafrika suala la uzazi linathaminiwa sana kwa sababu mimba huonekana kuwa ni baraka kutoka kwa miungu au Mungu (Magesa, 1997). Vilevile, uwezo wa kuzaa mtoto ni kitu muhimu katika ndoa. Pia, ndoa ni kigezo cha hadhi katika jamii. Aidha, kwa upande mwingine, uzazi ni njia ya kuendeleza mduara wa maisha katika (Wiredu,

---

[23]Ulimwengu wenye nyuga tatu hujumuisha ardhi wanayoishi watu, mizimu na viumbe wengine, kuzimu wanakoishi mizimu au wahenga na juu mbinguni anakoishi Mungu na miungu (Mulokozi, 2017).

[24]Uyakinifu wa kipragmatiki ni mtazamo wa kujali zaidi hali na mahitaji ya maisha ya sasa au yajayo na kujali vitendo kuliko nadharia. Maisha ya maana ni ya duniani si yale ya baada ya kufa (Mulokozi, 2017).

[25]Ujamiishaji wa kiduara ni mzunguko wa maisha toka kuzaliwa, kuota meno, unyago, kuoa/kuolewa, uzee, kufariki, kuwa mzimu na kuzaliwa tena (Mulokozi, 2017).

2006). Msingi huu umetuwezesha kueleza jinsi suala la uzazi linavyounda jaala za mashujaa wa tendi teule. Msingi mwingine ni nguvu ya kani. Msingi huu unafungamana na imani ya jamii za Kiafrika inayodai kuwa kila kiumbe kina kani uhai ambayo ni kiini cha kuwapo kwake. Kani hizi zinaweza kudhoofisha au kuimarisha maisha ya binadamu. Kani hizi huathiri kila kiumbe kulingana na nafasi yake. Mungu ndiye mwenye nguvu uhai kuu na hushikilia nguvu uhai za viumbe wengine kwa viwango tofauti. Kiwango cha juu kabisa ni cha wahenga na mizimu ambao wapo karibu na Mungu. Mizimu na wahenga hutumiwa na Mungu kama matarishi na viunganishi kati ya Mungu na wanadamu. Kwa hiyo, binadamu humfikia Mungu kwa njia ya wahenga (Tempels, 1945; Mbiti, 1969; Magesa, 1997; Nkemnkia, 1999; Mihanjo, 2004). Vilevile, kuna kani ya uganga, sihiri na uchawi. Katika jamii za Kiafrika, uganga na sihiri ni vipengele vya kiontolojia vinavyotumika kutatua matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii (Ilomo, 2013; Mpalanzi, 2019). Kwa upande mwingine, uchawi ni kani ovu zenye uwezo wa kuleta madhara kama magonjwa au vifo kwa binadamu (Mair, 1969; Chuachua, 2016). Katika makala hii msingi huu umebainisha kani mbalimbali zinavyochangia kuunda jaala za mashujaa.

Msingi wa uanthropomofia unahusu kumtanguliza binadamu; imani katika miviga, mizimu na miungu inayomhudumia mwanadamu katika mzunguko wa kuwapo hapa duniani (Mulokozi, 2017). Aidha, Mulokozi anaendelea kueleza kuwa kuheshimu wahenga hufanywa kwa njia ya matambiko ambapo wahenga hukumbukwa kwa majina katika tambizi, kutambikiwa na kuombwa msaada pale inapobidi. Mbiti (1991) anafafanua kuwa kufanya tambiko na kutoa sadaka hufanyika katika jamii nyingi za Kiafrika. Kupitia kitendo hiki ulimwengu unaoonekana na usioonekana hukutana na kuakisi malengo ya mwanadamu katika ulimwengu usioonekana. Tambiko hufanywa wakati maisha ya watu yako hatarini kwa lengo la kuwaokoa na kuweka ulinzi. Msingi huu umetumika kueleza mchango wa imani za kijadi katika kuunda jaala za mashujaa wa tendi teule.

Msingi wa mwisho ni umoja, mshikamano na uhusiano wa vilivyomo na maumbile. Wabantu wanashikilia kwamba kuna uhusiano kati ya viumbe na

muumba wao. Viumbe daima hushawishiana, huvutiana na kushirikiana kwa kukusudia au kutokukusudia na kusaidiwa na nguvu zisizo za kibinadamu au mababu. Wazo la Mwafrika la nguvu ni pamoja na mambo yote ya kimwili na kiroho. Mtu hawezi kuishi peke yake; lazima awe na uhusiano na nguvu nyingine zinazomuathiri pande zote, juu na chini katika mfumo wa ngazi zote za nguvu na uhai (Mihanjo, 2004). Misingi iliyofafanuliwa imetumika kufafanua vipengele vinavyounda jaala ya mashujaa katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha*. Misingi hii imetuwezesha kuchambua vipengele vya kiontolojia vinavyounda jaala za mashujaa kwa sababu inafungamana na ontolojia ya jamii ya Wahaya.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Maktabani, mtafiti alikusanya data kutoka katika makavazi ya TATAKI na Maktaba Kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mbinu ya uchanganuzi wa matini ilitumika kukusanya data zinazopatikana katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha* uliopo katika kitabu cha *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance* kilichoandikwa na Mulokozi (2002). Pia, tumedurusu vitabu, makala, na tasnifu zinazohusu masuala ya tendi pamoja na masuala ya ontolojia ya Kiafrika. Kwa upande wa uwandani, mtafiti ametumia njia ya mahojiano kukusanya data kuhusu vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vinavyojitokeza katika utendi wa *Rukiza*. Mahojiano yalihusisha watu waliopo katika mkoa wa Kagera, wilaya za Bukoba Vijijini, Missenyi na Muleba. Mahojiano yalihusisha sampuli ya watoa taarifa 20. Sampuli hiyo ilijumuisha wapiga nanga 10, wazee 8 na vijana 2. Sampuli hii iliteuliwa kwa sababu inafahamu tendi zilizochunguzwa na ontolojia ya jamii ya Wahaya. Data za maktabani na uwandani zimetuwezesha kufafanua vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vinavyounda jaala za mashujaa katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha*.

## 4.0 Vipengele Vinavyounda Jaala za Mashujaa katikaUtendi wa *Rukiza* na *Mugasha*

Jaala za mashujaa zinafungamana na mfumo mzima wa maisha ya shujaa tangu kuzaliwa hadi hatima yake. Katika sehemu hii tumefafanua vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vinavyounda jaala za mashujaa katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha*.

### 4.1 Kuthamini Uzazi

Kuthamini uzazi ni miongoni mwa vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vyenye umuhimu mkubwa katika kuunda jaala za mashujaa katika utendi teule. Katika jamii za Kiafrika uzazi huthaminiwa sana kwa sababu mimba huonekana kuwa ni baraka kutoka kwa miungu au Mungu (Mbiti, 1969; Magesa, 1997; na Kajosi, 2013). Baraka hizi zina umuhimu kwa wazazi na jamii. Kwa mfano, katika jamii za Kiafrika kama vile jamii za kitamaduni zinazopatikana huko Ghana watu huamini kuwa umuhimu wa watoto katika ndoa ni kigezo cha hadhi katika jamii, njia ya kuongeza ukoo na kuendeleza mduara wa maisha unaotuwezesha kuwapo (Wiredu, 2006). Vilevile, uzazi ni njia ya uzima wa milele yenye kuashiria umuhimu wa binadamu na ugumba ni laana na utupu kwa binadamu. Katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha*, thamani ya uzazi inajidhihirisha wakati wa kuzaliwa kwa mashujaa Rukiza na Mugasha. Kuna maajabu mengi yaliyoambatana na kuzaliwa kwao. Mathalani, katika utendi wa *Rukiza* shujaa akiwa tumboni alimweleza mama yake kuwa anazaliwa na jina lake aitwe Rukiza. Vilevile, Rukiza alieleza kuwa jaala yake ni kustawisha jamii ya Baganga na kurejesha utawala wa baba yake. Pia, shujaa alimwelekeza mama yake awaite Baganga kwa sababu anataka kuzaliwa. Mama yake alipomaliza kutekeleza yale aliyoambiwa, chupa ikapasuka. Mwandishi anaonesha suala hili katika beti zifuatazo:

20 *Ati "Oyalil'enju nk'egi*
*Mbwenu osbuntame onzale*
*Olankeleleza ndakubalukila*
*omulubunda!" Ai "Nazalwa*
*ndi Rukiza Rukiza eilembo*
*ly'Abaganga eli"*

20 Tandaza majani ya kukalia
sebuleni
Kisha keti unizae
Ukinichelewesha nitakupasukia
tumboni! Akasema, "ninazaliwa,
ndimi Rukiza
Rukiza mkombozi wa kaya hii ya
Baganga

*Kai "Mawe banza oiluke bwangu Onyetele Abaganga aho!*
*[Kandi kazilo omwana yazailwe*
*Kugila ati "Kantume omwana"*
*Manti niwe ainawe omw'ibunda]*
*Inya kazilo!*

Nenda kwanza uwaite Baganga!
[Maskini mtoto bado hajazaliwa
Hivyo, hakuna mtoto wa kumtuma
Maana mtoto ndiye yule aliyemo tumboni
Yarabi maskini!

*Rukiza mbona yabateka omw'ibanga*
*Ai "Baganga nazalwa*
*Naija kuzwala ndi Rukiza*
*Eibala lyange munyete Rukiza"*
*Ai "Kyonka inye kandazalwa*

Nikaona Rukiza anawakusanya sebuleni
Akasema "Baganga mimi ninazaliwa
Karibu nitazaliwa, ndimi Rukiza
Jina langu niiteni Rukiza"
Ila nitakapozaliwa

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 324 na 326)

Katika dondoo hii tunaona kuwa shujaa hata kabla ya kuzaliwa alishatambua jina lake. Pia, alifahamu kuwa jaala yake ni utawala na kuistawisha jamii ya Baganga. Umaizi huu si wa kawaida kwa watoto waliopo tumboni. Vilevile, kitendo cha shujaa kuzungumza akiwa tumboni si cha kawaida. Halikadhalika, utambuzi wa kuwapo kwa Baganga wakati hajawaona wala kuishi nao unadhihirisha kuwa umaizi wake ni tofauti na watoto wa kawaida. Kwa upande wa utendi wa *Mugasha*, kuzaliwa kwa shujaa Mugasha kuliambatana na maajabu yafuatayo:

*Ogye ojunge omulamba*
*Ogye ochwe enshankala*

Uende utengeneze juisi ya ndizi walipoikamua

| | |
|---|---|
| *Oiye obunyasi onzale 'nye*<br>*Ngye kujuba 'nye!" Yaleba*<br>*yashobelwa* | Uende ukate majani makavu ya<br>mgomba ukate na nyasi halafu<br>unizae!<br>Niende kuvua (samaki)<br>Akapigwa na butwaa |
| *Kandi nashobelwa Nikabona*<br>*mawe yanzala Kyonka*<br>*yayalama nye." Ai "Mawe*<br>*yanzala Yayalama* | Nikawa na wasiwasi<br>Naona mama amenizaa<br>Lakini amekosa chakula cha<br>mzazi." Akasema "Mama<br>amenizaa<br>Lakini amekosa chakula |
| *Ngende ngye mujubile*<br>*akafuru." Agenda nailuka*<br>*Agya aha mwalo si*<br>*Ogwabo ogwa Nyakilembeka*<br>*aaaa bwangu*<br>*Akatwa obubale eeee* | Hebu niende nikakuvulie<br>kijisamaki."<br>Akaenda akikimbia<br>Akaenda mwaloni<br>Mwalo wa kwao wa<br>Nyakilembeka aaaa haraka<br>Akachukua chambo |
| *Alob'enshato oooo*<br>*Alob' emumi*<br>*Akebela akabojo*<br>*Azileta*<br>*Ai "Mawe, nabona wanzala* | Akaloba sato<br>Akaloba mumi<br>Akageukia mbojo mdogo<br>Akawaleta<br>Akasema, "Mama naona<br>umenizaa |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:228, 243 na 244)

Nukuu hiyo inaonesha kuwa shujaa tangu akiwa tumboni alikuwa na uwezo wa kutambua mambo ambayo mama yake anapaswa kuyatekeleza ili azaliwe. Pia, shujaa akiwa tumboni alimwelekeza mama yake vitu anavyotakiwa kuviandaa ili aweze kuzaliwa. Vilevile, shujaa baada ya kuzaliwa aliweza kubaini kuwa mama yake ana njaa. Hata hivyo, hakuishia hapo alitafuta suluhisho la tatizo hilo kwa kwenda kumvulia samaki. Umaizi

huo unadhihirisha kuwa akili ya shujaa inatofautiana na watoto wengine. Pia, kitendo cha shujaa kukimbia baada ya kuzaliwa kinampa Mugasha sifa ya pekee ukilinganisha na watu wengine. Katika tendi hizi tumebaini kuwa kuzaliwa kwa mashujaa si kwa kawaida kwa sababu kuliambatana na mambo ya kipekee. Mashujaa walibobea katika matumizi ya lugha toka wakiwa tumboni na baada ya kuzaliwa. Hii ni kwa sababu mashujaa waliweza kutumia lugha sanifu kueleza mambo ya msingi ambayo hayategemewi kusemwa na watoto wachanga kutokana na uwezo wao wa akili. Kitendo hiki kinasigana na hatua za mtoto kupata na kubobea katika matumizi ya lugha. Watoa taarifa walipohojiwa kuhusu sababu ya kuwapo kwa maajabu wakati wa kuzaliwa kwa mashujaa walisema:

> Katika jamii yetu maajabu ya kuzaliwa yalijitokeza wakati wa kuzaliwa kwa machifu au wafalme. Mtoto akizaliwa akiwa ameshika kahawa au ulezi katika mkono wa kulia na mkono wa kushoto, wakunga walifahamu kuwa atakuwa mfalme ambaye atamrithi baba yake. Watoto wa machifu huzaliwa katika hali hiyo kwa sababu mizimu huwa imewachagua, hivyo, inadhihirisha suala la ufalme toka kuzaliwa kwao. Ndiyo maana kunakuwa na maajabu katika kuzaliwa kwao
> **Chanzo: (**Mahojiano na Mtoataarifa Na. 1, Tarehe 13/4/2020).

Nukuu hii inadhihirisha kuwa maajabu ya kuzaliwa si suala geni katika jamii ya Wahaya. Kiontolojia maajabu haya yalijitokeza kwa watoto wa machifu ambao wameteuliwa na mizimu kurithi tawala za baba zao. Hivyo, maajabu ya uzazi katika jamii ya Wahaya yanafungamana na watu wenye jaala ya utawala. Lord (1991) anaunga mkono suala hilo kwa madai kuwa kuzaliwa kwa mashujaa huelezea sifa zao maalumu. Matendo anayofanya kipindi cha utoto yanatoa mapema ushahidi wa mwonekano, nguvu za ziada na asili yake ambayo ni ya tofauti. Kwa muktadha huo, mashujaa wa tendi za *Rukiza* na *Mugasha* wamefungamana na maajabu ya uzazi kwa sababu

walikuwa na asili ya utawala toka kwa baba zao. Kwa mantiki hiyo, maajabu hayo katika ontolojia ya Wahaya yalidhihirisha kuwa mashujaa wana jaala ya utawala. Okpewho (1979) na Mulokozi (2002) wanaunga mkono suala hili kwa madai kuwa jaala ya shujaa inaanzia utotoni na kukua kwake si kwa kawaida. Suala hili linasababisha kuzaliwa kwa shujaa kuhusishe matukio makubwa na maajabu ambayo hayajawahi kujitokeza katika maisha ya watu wa kawaida. Okpewho anaendelea kueleza kuwa matukio hayo humtofautisha shujaa na watu wengine na kuweka msingi wa jaala yake. Kwa mantiki hiyo, katika ontolojia ya jamii ya Wahaya thamani ya uzazi si baraka, heshima na kuendeleza ukoo peke yake. Katika tendi za *Rukiza* na *Mugasha* tumebaini kuwa kipengele cha uzazi ni njia inayotumiwa na mizimu kudhihirisha jaala ya utawala kwa mashujaa wa tendi teule. Vilevile, maajabu yanayoambatana na uzazi yamewatofautisha mashujaa na watu wengine kwa lengo la kujenga msingi wa jaala zao za utawala. Hivyo, kipengele cha uzazi kimechangia kuunda jaala za mashujaa wa tendi teule toka wakiwa wadogo.

## 4.2 Nguvu ya Kani

Mashujaa wa tendi za Nanga wanafungamana na kani za kimwili, kiakili na nguvu za mizimu au sihiri (Mulokozi, 1986). Kani za kimwili na sihiri zimejitokeza kwa namna mbili katika tendi za *Rukiza* na *Mugasha*. Katika utendi wa *Mugasha,* sihiri ya shujaa imehifadhiwa katika mwili wake. Kwa upande wa utendi wa *Rukiza*, sihiri ya shujaa imehifadhiwa kwenye vyanzo vyake vya sihiri. Utendaji wa kani za sihiri umefungamana na nguvu za kimwili za mashujaa. Kani za kimwili na sihiri zimejidhihirisha kupitia vitovu vya mashujaa na matendo ya mashujaa. Wakati wa kuzaliwa kwa mashujaa, wakunga hawakufanikiwa kukata vitovu vyao kwa kutumia vifaa vya kawaida kama mwanzi, wembe na kisu. Kitovu cha Rukiza kilikatwa kwa kutumia shoka na kitovu cha Mugasha kilikatwa kwa kutumia mgomba wa *ntembe*. Sababu ya matumizi ya vifaa hivyo katika ukataji wa vitovu vya mashujaa imewasilishwa katika maelezo yafuatayo:

> Mgomba wa *ntembe* ni mgomba ambao unazaa ndizi ambazo ndani yake hazina ndizi bali huwa na vitu vyeusi

> vinavyoitwa *ntembe*. Mgomba huo hutumiwa na waganga wa jadi kufanya ubashiri na kutoa matibabu kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na mapepo au uchawi. *Ntembe* huchanganywa na dawa nyingine na kutengeneza hirizi ambayo huwekwa chini ya mto ili mchawi akija asiweze kukuona. Mgomba huu ni wa mizimu. Ukikuta mgomba huu umeota mahali ujue mahali hapo kuna *mbandwa*. Shoka au *mbeizo* ni kifaa ambacho kinatumika katika matambiko ya jadi. Kifaa hiki hutumika kutengenezea nanga, mitumbwi, na vifaa vingine. Wazee walipokuwa wanafanya matambiko wakati mwingine walikitumia katika shughuli za matambiko
> **Chanzo:** (Mahojiano na Mtoataarifa Na. 8, Tarehe 5/5/2020).

Maelezo hayo yanathibitisha kuwa shoka na mgomba wa *ntembe* ni vifaa vya kiganga. Vifaa hivyo hutumika katika shughuli za kiganga kama ubashiri na matambiko. Kutokana na majukumu yake ni dhahiri kwamba vifaa hivi vinafungamana na nguvu za mizimu. Aidha, vifaa hivyo vilifanikiwa kukata vitovu vya mashujaa kwa sababu vina kani za mizimu zinazoendana na miiko inayofungamana na nguvu za sihiri zilizopo katika miili ya mashujaa. Katika ontolojia ya jamii za Kiafrika, miiko hiyo huhusisha maarifa ya siri ambayo yanamwezesha shujaa kuishi katika ulimwengu wa watu wenye nguvu zaidi za kimwili (Deme, 2009). Ukiukwaji wa miiko inayofungamana na sehemu nyeti yenye sihiri ya shujaa huweza kusababisha kifo au kuanguka kwa shujaa (Lyamuya, 2014). Kwa mfano, katika utendi wa *Fumo Liyongo* shujaa hakuweza kudhurika kwa njia yoyote ila kwa kuchomwa sindano ya shaba kitovuni. Hapo ndipo penye nguvu zake; ndipo penye sihiri yake (Mulokozi, 1999). Kwa hiyo, ukiukwaji wa miiko inayofungamana na sihiri iliyopo katika mwili wa shujaa Liyongo ulisababisha kifo chake. Kutokana na muktadha huo, vifaa vilivyoweza kukata vitovu vya mashujaa vinaendana na miiko inayofungamana na sihiri iliyopo mwilini mwake. Hali hiyo imewawezesha

wakunga kukata vitovu vya mashujaa bila kuathiri uhai na sihiri yao. Katika ontolojia ya jamii ya Wahaya, maajabu yanayofungamana na vitovu vya mashujaa yanadhihirisha kuwa mashujaa wana nguvu za sihiri mwilini mwao. Vilevile, katika ontolojia ya jamii za Wahaya, kitovu ni kiini cha mafanikio ya binadamu. Kwa mantiki hiyo, maajabu yaliyofungamana na vitovu vya mashujaa ni njia inayotumiwa na mizimu kudhihirisha jaala za mashujaa.

Sihiri ya mashujaa imejidhihirisha kupitia matendo yao. Mashujaa wamefanya matendo mbalimbali ambayo yanadhihirisha kuwa wana nguvu za kimwili na za sihiri mwilini mwao. Kwa mfano, Rukiza na Mugasha waliweza kuzungumza tangu wakiwa tumboni. Rukiza baada ya kuzaliwa alikunywa kianzi kizima cha maziwa na Mugasha alitembea na kwenda kumvulia mama yake samaki. Rukiza alitumia mkojo na ushuzi wake kuwapofua macho Wanyambo na kufanikiwa kupita mwaloni na kuelekea Byantanzi. Pia, Rukiza alilipiga dume kubwa la ng'ombe la baba yake na kuliangusha kwenye moto kisha akalichinja kwa kutumia vidole. Halikadhalika, Mugasha aliweza kujenga nyumba kwa kutumia nguzo na tete moja. Vilevile, Mugasha alimpiga Kagoro Kemango na kumuingiza kwenye mwamba kisha akamtoa akiwa bubu. Matendo ya mashujaa hawa yameelezwa katika beti zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 75 | *Engabizo zo'mwana*<br>*Obukankabana nabwanga*<br>*Mugende omunte za tata"*<br>*Ai "Baganga kilo ekya mbwenu Mukame ekyanzi ndakinywa* kyona" | 75 | Ama kuhusu lishe ya mtoto<br>Visumba vya ndizi navikataa<br>Nendeni katika ng'ombe wa baba<br>Baganga siku hii ya leo<br>Kamueni kianzi kizima cha maziwa nitakinywa chote |
| 110 | *Yagitela akatome omw'ibunda*<br>*Nkabona enumi aha komiyangw'entule*<br><br>*Eeeee ai bambi!* | 110 | Akampiga dume kigumi chake<br>Nikaona dume huyo anaanguka mweleka karibu na moto<br>Eeee ai siku hiyo! |

*Bai “Iloko mulete emihyo”*
*Bagya kubiga emihyo*
*Abaganga*

Wakasema, “Nendeni mlete visu”
Baganga wakaenda kutafuta visu

*Baganga kagibaga n’ebyala!*
*Bakashanga kabagile kalile!*
*Bai “Ti kana twabona eiyembe!”*
*Rukiza kilekyo yatuula*
*Ai “Baganga mbagambile*

Waliporudi walikuta kimekwisha
mchinja dume kwa vidole vyake
Walikuta kimekwishamchinja na kula nyama
Wakamaka huyu si mtoto tumeona kioja!
Siku hiyo Rukiza akatamakani
Akasema,” Baganga hebu niwaambie

*Ai “Bunyambo, nakubaisize*
*amachumu*
*Tinyina mukaikulu alagogya*
*Nakubalasile nemyambi yange*
*egi Tinyina mukaikulu*
*alagyogya!” Omwana mbona*
*yanyala enkai*

Akasema, Vinyambo
ningewaua kwa
mikuki yangu
Lakini sina ajuza wa kuuosha
Ningewarushia mishale yangu hii
Lakini sina ajuza wa kuiosha
Hapo nikaona mtoto anakojoa mkojo

*Nkabona echuuchuyabwigala*
*amaisho! Kayanyampile*
*ekinyampo kyonka*
*Obunyambo eshaabo*
*yabuhoma amaisho!*
*Obunyambo buti “Mulugize*

Nikaona vumbi linavipofusha macho!
Alipojamba tu
Vumbi likavikandika machoni!
Vinyambo vikasema
“Mpisheni aende! Mtoto huyu

| | |
|---|---|
| *agende! Omwana ogu twashabula eiyembe ekikuniila!”* | tumevusha kioja, ndumba! |

**Chanzo: (**Mulokozi, 2002: kur. 326-333)

| | |
|---|---|
| *Kandi nashobelwa*<br>*Nikabona mawe yanzala*<br>*Kyonka yayalama nye.”*<br>*Ai “Mawe yanzala*<br>*Yayalama* | Nikawa na wasiwasi<br>Naona mama amenizaa<br>Lakini amekosa chakula cha mzazi.”<br>Akasema “Mama amenizaa<br>Lakini amekosa chakula |
| *Ngende ngye mujubile akafuru.”*<br>*Agenda nailuka*<br>*Agya aha mwalo si Ogwabo ogwa Nyakilembeka aaaa bwangu*<br>*Akatwa obubale eeee* | Hebu niende nikakuvulie kijisamaki.”<br>Akaenda akikimbia<br>Akaendwa mwaloni<br>Mwalo wa kwao wa Nyakilembeka aaaa haraka<br>Akachukua chambo |
| *Alob’enshato oooo*<br>*Alob’ emumi*<br>*Akebela akabojo azieta*<br>*Azileta* | Akaloba sato<br>Akaloba mumi<br>Akageukia mbojo mdogo<br>Akawaleta |
| *Bahamweleka aaaa*<br>*Bagya bamweleka olukeeko*<br><br>*Ayombeka Ilemeile*<br>*Akatema enyomyo emwoi*<br>*Yayombeka enju yagimala* | Wakamwonesha mahali aaaa<br>Wakaenda wakamwonyesha sehemu ya kujenga<br>Akajenga mwenye mashavu manene ya miguu<br>Alikata nguzo moja<br>Akajenga nyumba ikaisha |
| *Ilemeile, Nshag’ Omuhanda*<br>*Olubingo lumwoija* | Nfundo Nene, Mpana kuzidi<br>Njia |

| | |
|---|---|
| *Baleba bashobelwa*<br>*Ekyegile eeee!*<br>*Kimwe, bibili, bishatu binai* | Alitumia utete mmoja<br>Wakaangalia kwa mshangao<br>Maajabu hayo!<br>Moja, mbili, tatu nne |
| *Ati "Yayetwala Kagoro!"*<br>*Ai "Kanyegendele eeee*<br>*Tintume ntumwa ni zingi!"*<br>*Aija nailuka muno bwangu*<br>bwangu N'okugulu kumwe | Akasema amejitawala Kagoro!<br>Akaema "Hebu niende<br>mwenyewe eeee Sitatuma<br>wajumbe wengine!"<br>Akaja anakimbia wangu<br>wangu Na mguu mmoja |
| *Yatela aha lwazi*<br>*Lwayashama*<br>*Lwashuba lwabumba!*<br>*Bai "Leka" "Bai Leka!"*<br>*oooo*<br>*Bai "Leka, lamulwa!* | Akambamiza kwenye<br>mwamba<br>Mwamba ukafunguka<br>Kisha ukajifunga!<br>Wakasema "Basi" "Wakasema<br>"Basi" oooo Wakasema<br>"Acha, kubali suluhu! |
| *Atela aha lwazi Alugamu*<br>*Alugamu nahebebela bu bu*<br>*bu bu bu bu!*<br>*Ni Kemango*<br>*Olulimi lwakubile* | Akagonga kwenye mwamba<br>Kagoro akatoka<br>Lakini akatoka akiropoka: Bu<br>bu bu<br>bu bu!<br>Ni Kemango<br>Ulimi umekwisha nasa |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:228-289)

Mashujaa waliweza kutenda matendo makubwa kinyume na umri wao na uwezo wao wa kiakili kwa sababu wana nguvu za kimwili, kiakili na nguvu za sihiri. Suala hili linajidhihirisha kupitia kitendo cha Rukiza na Mugasha kuzungumza tangu wakiwa tumboni. Kibiolojia, mtoto akiwa tumboni huwa

na uwezo wa kuwasiliana na viumbe wengine walioko nje kwa njia ya hisia lakini hawezi kuzungumza nao. Hali hii huanza kujitokeza katika kipindi cha wiki ya 14 hadi wiki ya 20. Katika kipindi hiki mtoto huanza kukabiliana na mazingira yake na husikia sauti tofauti ambazo zinatoka nje ya mfuko wa uzazi (Cobb, 2001). Kwa hiyo, kitendo cha mashujaa kuzungumza wakiwa tumboni ni cha kipekee na kinadhihirisha kuwa nguvu za sihiri ndizo zilizowawezesha kutenda mambo hayo. Kimsingi, nguvu hizi zinatokana na kani uhai ambayo hata wao wenyewe hawana mamlaka nayo bali wamezaliwa nayo kiasili. Vilevile, shujaa Mugasha baada ya kuzaliwa aliweza kutembea na kwenda kuchukua mtumbwi, kisha akaingia ziwani kumvulia mama yake samaki. Kibiolojia, mtoto ili aweze kutembea huanza kulala chini, kutambaa, kukaa, kusimama, kutembe huku kashikilia kitu kisha huweza kutembea (Carlson na Buskist, 1997). Kitendo cha Mugasha kutembea baada tu ya kuzaliwa kinasigana na maendeleo ya mtoto kulingana na hatua anazotakiwa kupitia mpaka aweze kutembea. Kiontolojia, uwezo wa shujaa kutembea kabla ya kipindi chake unafungamana na kani za sihiri zilizopo mwilini mwake ambazo huaminika kuwa zinatokana na majaliwa kutoka kwa Mungu.

Katika hali ya kawaida mkojo na ushuzi wa binadamu hauwezi kutimua vumbi na kupofusha watu macho. Kitendo cha mkojo na ushuzi wa Rukiza kuwafunika na kuwapofua macho Wanyambo kinadhihirisha kuwa takamwili hizo zina kani za ziada. Aidha, mwili wa shujaa Rukiza una nguvu za sihiri; kwa hiyo, hata takamwili zilizotoka katika mwili wa shujaa zina nguvu za sihiri. Shujaa akafanikiwa kutumia takamwili kama silaha ya kupambana na adui zake. Vilevile, shujaa Mugasha aliweza kujenga nyumba ya kijadi kwa kutumia nguzo na tete moja. Kitendo hiki kinadhihirisha kuwa shujaa ana nguvu za sihiri zinazomwezesha kuongeza nguzo na matete aliyoyatumia katika ujenzi. Pia, si rahisi kwa mtu mmoja kufanikiwa kujenga nyumba ya kijadi. Muundo wa nyumba za kijadi huwalazimisha watu kushirikiana katika ujenzi. Kitendo cha shujaa kujenga nyumba hiyo peke yake kinadhihirisha kuwa alitumia nguvu za sihiri katika ujenzi huo. Vilevile, sihiri inajidhihirisha kupitia kitendo cha shujaa kufanikiwa kupiga dume la ng'ombe ngumi na kuliangusha kwenye muoto wa watoto. Katika hali ya kawaida ngumi ya mtoto mdogo haiwezi kupiga dume la ng'ombe na kuliangusha. Kitendo hiki kinadhihirisha kuwa ngumi hiyo imefungamana na kani za sihiri zilizopo

mwilini mwa shujaa. Vilevile, katika hali ya kawaida mtu akitaka kumchinja ng'ombe lazima atumie vifaa kama kisu, panga au shoka. Kitendo cha Rukiza kuchinja dume la ng'ombe kwa kutumia vidole kinadhihirisha kuwa kuna kani za sihiri katika vidole vyake zilizomwezesha kuchinja dume hilo.

Katika utendi wa *Mugasha* kani za sihiri zimejitokeza kupitia kitendo cha shujaa kumbamiza Kagoro kwenye mwamba, mwamba kufunguka, Kagoro kutumbukia humo kisha mwamba ukajifunga. Kitendo hiki kinadhihirisha kuwa kuna nguvu za sihiri zilizotumika kufungua mwamba na kusababisha Kagoro atumbukie humo, kisha mwamba ukajifunga. Kwa kawaida mwanadamu hawezi kuwa na kani ya kupiga na kufungua mwamba. Vilevile, mwamba ukijifunga hauwezi kujifungua wenyewe. Halikadhalika, nguvu za sihiri zinajidhihirisha kupitia kitendo cha Mugasha kupiga mwamba na Kagoro kutoka akiwa hai. Kwa hali ya kawaida mwamba ukijifunga hatuwezi kuufungua kwa kuupiga. Kwa hiyo shujaa ametumia kani za sihiri kuufungua mwamba ili Kagoro Kemango aweze kutoka. Vilevile, kibiolojia binadamu hawezi kuishi ndani ya mwamba kwa sababu hakuna hewa. Kitendo cha Kagoro Kemango kutoka ndani ya mwamba akiwa bubu badala ya kuumia viungo vyake kinadhihirisha kuwa tukio hilo linafungamana na nguvu za sihiri.

Katika tendi za *Rukiza* na *Mugasha* matukio ya kisihiri yanayoambatana na kuzaliwa kwa mashujaa ni njia iliyotumiwa na mizimu kudhihirisha jaala yao ya utawala. Vilevile, mashujaa waliweza kutumia nguvu zao za sihiri kufanya matendo mbalimbali. Nguvu hizo zimewawezesha kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri, kutambua jaala zao na kutatua vikwazo mbalimbali walivyokutana navyo katika msako wa jaala zao. Vilevile, nguvu za sihiri zimetoa mchango mkubwa katika matukio ya kipekee yaliyotendwa na shujaa. Matukio hayo yanawatofautisha mashujaa na watu wengine. Yamedhihirisha jaala yao ya utawala na kuwawezesha kutatua changamoto mbalimbali walizokabiliana nazo katika msako wa jaala zao. Hivyo, mashujaa wanahitaji kani za kimwili na sihiri katika kuunda jaala zao.

## 4.3 Kuheshimu Wahenga

Katika ontolojia ya jamii za Kiafrika kuheshimu wahenga au mahoka hufanywa kwa njia ya matambiko ambao hukumbukwa kwa majina katika tambizi, kutambikiwa na kuombwa msaada pale inapobidi (Mulokozi, 2017). Katika utendi wa *Rukiza*, shujaa aliwaheshimu wahenga kwa kutoa tambiko lililohusisha kafara ya mtwana. Watu walipohoji sababu za kumuua mtwana, shujaa akawaambia kuwa ametoa sadaka kwa lengo la kunusuru kaya ya Baganga na umaskini. Tazama maelezo ya suala hili katika nukuu na beti zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 165 | *Keyagobile omwabo*<br>*Byantanzi Ndwo*<br>*yabugangainwe omwiru*<br>*Yananuula emyambi*<br>*bwankyai mbona*<br>*yamwita! Bai "Rukiza*<br>*nka waita omwiru?"*<br><br>*Ati "Ekyo kitambo*<br>*kyomwaitu!"* | 165 | Alipofika Byatanzi<br>Ndipo alipokutana na mtwana<br>Akavuta upinde asubuhi na<br>kumwua kwa mshale!<br>Watu wakauliza, "Rukiza mbona<br>Umemwua mtwana?"<br>Akajibu, "Hiyo ni sadaka ya kaya<br>yetu" |

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 332-334)

Nukuu hii inadhihirisha kwamba tambiko la mtwana lina umuhimu mkubwa katika kuunda jaala ya ustawi wa jamii ya Baganga. Katika ontolojia ya Wahaya matambiko yanafungamana na dini ya jadi. Tambiko la mtu lilifanywa na machifu kipindi cha zamani. Tambiko hili lilihusisha kafara ya mtwana kwa sababu ni mtu/watu wa tabaka la chini. Watoa taarifa walipoulizwa sababu ya kutoa tambiko la mtwana, mmoja wao alisema:

> Tambiko katika jamii ya Wahaya ni njia mojawapo ya kuwafikia wahenga. Matambiko hutolewa katika jamii ya Wahaya kwa ajili ya kutatua changamoto za watu binafsi na za jamii. Kwa upande wa matatizo ya kijamii tambiko hutolewa kutatua matatizo kama vile njaa, ukame,

> mafuriko, wadudu au magonjwa. Aidha, matambiko ya watu binafsi yanahusu masuala ya ndoa, kutopata mtoto, mafanikio ya mtu binafsi na kutoa shukrani. Matambiko binafsi na ya kijamii yanahusisha sadaka ya ngombe, kondoo, mbuzi, pombe na kahawa. Tambiko la mtu lilifanywa mara chache kwa ajili ya kutatua matatizo ya jamii nzima kutokana na maelekezo ya mizimu. Mukama aliagiza mtu huyo atolewe sadaka mfano kwenye ziwa au porini kwenye tingatinga. Watu walikuwa wanauliwa ili watu wengine wapone. Matambiko yalikuwa ni sehemu ya dini za jadi
> **Chanzo**: (Mahojiano na Mtoataarifa Na. 14, Tarehe 10/4/2020)

Nukuu hizo zinadhihirisha kuwa katika jamii ya Wahaya matambiko yalihusisha wanyama, sadaka za vitu mbalimbali na binadamu. Tambiko la kafara ya binadamu lilifanywa mara chache katika kipindi cha utawala wa wafalme na machifu. Kafara hizo zilitolewa wakati wa ujenzi wa ikulu ya mfalme, ziwani au porini. Katika jaala ya shujaa Rukiza, kafara ya mtwana ililenga kutatua matatizo ya jamii nzima. Hali hiyo ndiyo iliyomfanya Rukiza atoe sadaka ya mtwana kwa lengo la kuiponya jamii ya Baganga na umaskini. Rukiza alichagua tambiko la mtwana kwa sababu katika ontolojia ya jamii za Kiafrika tambiko la damu hurudisha maisha ya mwanadamu kwa Mungu ambaye kwa uhalisia ni chanzo cha maisha yote (Mbiti, 1991). Kwa hiyo, tambiko ni njia iliyomwezesha shujaa kuungana na mizimu katika utatuzi wa changamoto ya umaskini ulioigubika jamii yake. Kwa upande mwingine, tambiko lilimwezesha shujaa kuweka ulinzi katika kaya mpya aliyoianzisha eneo la Byantanzi. Pia, wahenga waliwezesha jamii ya Baganga kumiliki mifugo ya kutosha iliyowapatia maziwa na samli. Kwa upande mwingine, katika utendi wa *Mugasha*, kuheshimu wahenga kulimwezesha Kajubi kutatua tatizo la kukosa mtoto. Kajubi alitoa sadaka ya tisini na tisa kuomba mizimu imsaidie kutimiza jaala ya kumzaa

Mugasha.Vilevile, wakati shujaa anazaliwa watu walitoa sadaka ya tisini na tisa kwa mganga ili watambue kifaa cha kukatia kitovu cha shujaa.

| | |
|---|---|
| *Bagya bamutelela amaizi*<br>*Bati “Kyonka iwe Kajubi eya Kajubi*<br>*Noija kugya kuzala*<br>*Kyonka olizala wafiile*<br>*Otakimanya kantu* | Wakaenda wakapiga ramli ya maji<br>Wakasema, “Lakini wewe Kajubi wa Kajubi<br>Utakuja kuzaa<br>Lakini utazaa umekwishafariki<br>Bila fahamu tena |
| *Mara noija kuzala omwana*<br>*Mbaija kumuha eibala*<br>*Mbaija kumweta Mugasha”*<br>*Yaiyaho ekyende na mwende*<br>*Yagaluga-aaaa* | Hakika utakuja kuzaa mtoto<br>Watamwita jina<br>Watamwita Mugasha.”<br>Akatoa tisini na tisa<br>Akarudi- iiii |
| *Baihamu ekyende n’omwende aaaa Yoooo!*<br>*Bagya Kikuku omwa Ibagwa oo lya Kagengele*<br>*Enyege yaikwata aaaa*<br>*Ekitebe yakikalila*<br>*Yatela enyimba yagamba* | Wakachukua tisini na tisa yoooo!<br>Wakaenda Kikuku kwa Ibagwa oo wa Kagengele<br>Akashika manyanga yake<br>Akakaa kwenye kiti chake<br>Akapiga manyanga ikasema |
| *Yatungamilwa*<br>*Ai “Mugende nimwiluka*<br>*Mugende nimwiluka*<br>*Mugye Kagoma omwa Nyamaizi*<br>*Mugye mwihemu ekyai Ky’entembe* | Akapandwa na mizimu<br>Akasema, “Nendeni mkikimbia<br>Nendeni mkikimbia<br>Nendeni Kagoma kwa Nyamaizi<br>Mchukue humo gamba la mgomba wa aina ya *ntembe* |

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 218-240)

Katika nukuu hizo tumeelezwa kuwa watu walipokwenda kwa mganga walitoa tisini na tisa. Katika ontolojia ya jamii ya Wahaya, tisini na tisa ni tambiko siyo ada. Kuhani wa dini ya kijadi akikupatia huduma hatozi ada bali mtu hutoa tambiko linalohusisha vitu tisa. Motifu ya tisa inatumika katika tambiko kwa sababu mizimu mikuu ilikuwa tisa. Unapotambika lazima upeleke vitu tisa ili kila mzimu upate. Mtu akitoa vitu tisa anafanikiwa katika mambo yake kwa sababu ameihusisha mizimu yote. Vilevile, katika ontolojia ya jamii ya Wahaya, tisini na tisa inaashiria upendo au kupendana. Watu wanaamini kwamba ukitoa tisini na tisa mizimu hupokea sadaka yako na utafanikiwa vizuri katika mambo yako. Hivyo, sadaka iliyotolewa kwa mizimu ilichangia kuunda jaala ya shujaa kwa sababu ilimwezesha mganga kuelezwa na mizimu kifaa kitakachokata kitovu cha shujaa na sehemu kinapopatikana. Watu wakafanikiwa kwenda Kagoma kwa Nyamaizi kuchukua gamba la mgomba wa *ntembe*. Gamba hilo likafanikiwa kukata salama kitovu cha shujaa. Vilevile, sadaka ya tisini na tisa imemwezesha Kajubi kutatua tatizo lake la uzazi na kutimiza jaala ya kumzaa shujaa Mugasha. Matambiko hayo yalitolewa kwa sababu katika ontolojia ya jamii za Kiafrika tambiko na sadaka humuunganisha binadamu na ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Mtu lazima atoe matambiko kwa miungu au mababu ili maisha yake yaweze kustawi (Mbiti, 2011; Ukwamedua na Omokpo, 2016). Hivyo, kupitia tambiko mashujaa walifanikiwa kuunda jaala zao kwa kupata nguvu za sihiri, kutatua changamoto ya kifaa cha kukatia kitovu cha shujaa, kuistawisha jamii na kuwapa ulinzi mashujaa na jamii zao. Kwa mantiki hiyo, kuheshimu wahenga kuliwawezesha mashujaa kutatua matatizo binafsi na ya kijamii, jambo lililowawezesha kutimiza jaala zao.

### 4.4 Umoja, Mshikamano na Ukamilisho wa Maumbile

Katika jamii za Kiafrika kuna uhusiano wa kiontolojia kati ya kiumbe mmoja na mwingine. Viumbe wote huungana na viumbe wengine kwa namna kwamba kila mmoja humuathiri mwenzake vibaya au vizuri. Hakuna kinachojongea katika ulimwengu bila kuathiriwa na kani uhai nyingine (Magesa, 1997). Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kuna ushikamani wa

kiontolojia kati ya binadamu na jamii yake. Mshikamano huo wa kiontolojia ndio unaowawezesha viumbe kuendelea kuishi na kutimiza jaala zao.

Katika tendi tulizochunguza, mashujaa wameshikamana na jamii, mizimu, wanyama na vitu mbalimbali katika msako wa jaala zao. Hii ni kwa sababu shujaa peke yake hawezi kutimiza jaala aliyopangiwa na Mungu. Kwa mfano, katika utendi wa *Mugasha*, shujaa alishirikiana na mizimu katika msako wa jaala ya utawala na jaala ya mwanamke. Kwa upande wa watu, shujaa ameungwa mkono na baba yake ambaye alikubali kufa ili shujaa Mugasha azaliwe. Vilevile, katika jaala ya uzazi, shujaa Mugasha ameungwa mkono na mama yake anayeitwa Nyambubi ambaye amewajibika kubeba mimba na kumzaa shujaa. Pia, wakunga walifanya maombi na kutafuta kifaa cha kukatia kitovu cha shujaa. Mambo haya yameelezwa katika beti zifuatazo:

*Bantelelela amaizi*
*Ngu kandigya kuzala omwana*
*Ninjakumuzala nafiile*
*Ntakimanya Kantu"*
*Ahi "Waihukayo"*

Wakanichapia maji
Wakaona kuwa nikija kuzaa
Nitazaa mtoto nimekwishafariki
Nitakuwa sitambui kitu."
Akasema pole na safari

*Yatungamilwa bwangu*
*Ahi "Mugende nimwiluka*
*Mutwale amagulu nk'empungu*
*muno muno*
*Mugye Kagoma ka Nyamaizi*
*Mugye mwiyemu omukaikulu*

Haraka akapandwa na mizimu
Akasema nendeni mkikimbia
Pelekeni miguu yenu mbio
mbio kama tai
Nendeni Kagoma kwa
Nyamaizi Mkamchukue Bi
Kizee hapo

*Omugenyi wa Kitangaza*
*Omugenyi wa bwaigolo*
*Agye azaze omwana*
*Nyenkya kandi agye kujuba."*
*Baija nibailuka muno*

Mgeni asiyetarajiwa
Mgeni wa jioni
Aje amzalishe mtoto
Ili kesho aende kuvua samaki."
Wakaja wakikimbia mno

*Wanene omukazi*
*Ahulila omunda*
*Ahulila ensisilo*
*Keyaimukile bwalukyakya*
*Keyaimukile bwalukyakya*

Na hapo yule mwanamke
Akajisikiliza tumboni
Akasikia mtikisiko
Alipoamka asubuhi na mapema
Alipoamka asubuhi na mapema

*Bwankyai bwalukyakya*
*Bwankyai bwalukyakya*
*Byalukyakya siii eeee*
*Balima enyanga ya Kajubi*
*Bwaigolo bazika Kajubi eya*
*Kajubi!*

Asubuhi na mapema
Asubuhi na mapema
Asubuhi na mapema siii eeee
Wakachimba kaburi la Kajubi
Jioni wakamzika Kajubi wa
Kajubi!

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 222-234)

Data za nukuu hii zinadhihirisha kuwa mafanikio ya jaala ya kuzaliwa kwa Mugasha yalitokana na ushirikiano wa Nyambubi, wakunga na Waganga. Kupitia uganga, mizimu ilieleza mtu ambaye angeweza kumzalisha mama yake Mugasha. Vilevile, mizimu ilieleza kifaa ambacho kingeweza kukata kitovu cha shujaa. Pia, katika mapambano, shujaa alishirikiana na mizimu ambayo ameitumia katika mfumo wa mawingu, mvua, radi na upepo. Shujaa alitumia upepo wa *Nkomaizi*, *Mushoke*, *Mbuyaga* na *Mwegundu*. Mugasha ametumia vitu hivyo kwa sababu katika ontolojia ya jamii za Kiafrika, tukiacha Mungu, kuna elementi za kiroho ambazo ziko katika ulimwengu usioonekana ambazo zinaathiri maisha ya mwanadamu. Kundi la kwanza ni roho ambazo ni binadamu na kundi la pili ni roho ambazo si binadamu na kuwapo kwake hakuhusiani na kitu chochote. Roho hizo

huchukua umbo la dunia au hewa, jua, mvua, mwanga wa radi na ngurumo za radi. Japokuwa roho hizo hatuzioni kwa macho, utendaji wake huhusishwa na matukio na hali zilizopo duniani (Magesa, 1997). Hivyo, katika utendi wa *Mugasha*, shujaa alitumia roho zisizoonekana katika mfumo wa maji, mawingu, upepo, mvua na radi. Roho hizo katika ontolojia ya jamii ya Wahaya zinahusishwa na Mugasha pamoja na mizimu mingine inayofungamana naye. Mizimu hiyo imetumiwa na shujaa kutekeleza majukumu mbalimbali katika mapambano ya msako wa jaala yake. Hivyo, ushirikiano wa Mugasha na mizimu ya anga katika mapambano ulimwezesha kutimiza jaala ya kumwoa dada yake Lyangombe na kurejesha utawala wa baba yake uliopo katika eneo la Sesse. Pia, Mugasha baada ya kutimiza jaala yake watu walisherehekea na kucheza ngoma za jadi. Hii ni ishara kuwa jamii iliunga mkono jaala ya shujaa Mugasha.

Katika utendi wa *Rukiza* kuna mshikamano wa kiontolojia kati ya shujaa, mizimu na jamii yake. Mshikamano huo unajidihirisha kupitia tambiko na sihiri ya shujaa. Shujaa alitumia tambiko la mtwana kuiomba mizimu isaidie jamii yake kuondokana na ufukara. Kupitia tambiko hilo maisha ya jamii ya Baganga yalistawi, watu wakaneemeka na kuondokana na ufukara. Tutazame jambo hili katika beti zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 165 | *Keyagobile omwabo<br>Byantanzi Ndwo<br>yabugangainwe omwiru<br>Yananuula emyambi<br>bwankyai mbona yamwita!<br>Bai "Rukiza nka waita<br>omwiru?"<br>Ati "Ekyo kitambo<br>kyomwaitu!"* | 165 | Alipofika Byatanzi<br>Ndipo alipokutana na<br>mtwana<br>Akavuta upinde asubuhi na<br>kumwua kwa mshale!<br>Watu wakauliza, "Rukiza<br>mbona umemwua mtwana?"<br>Akajibu, "Hiyo ni sadaka ya<br>kaya yetu!" |

| | |
|---|---|
| *Bamuketa ekikale bateela* | Wakatamakani naye na kumjengea kitala |
| *Aho nkabona obukama nk'obundi* | Ukawa ufalme kama falme nyingine |
| *Abaganga lyakila obwolo* | Baganga wakapona ufukara |
| *Banywa amata gayanga* | Wakanywa maziwa yakawashinda |
| *Agandi bagazanyia omw'ishazi* | Mengine wakayamwaga kwenye *Ishazi* |

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 332)

Beti hizo zinaeleza kwamba baada ya shujaa kutoa sadaka ya mtwana, kaya ya Baganga ilistawi. Suala hili linadhihirisha kuwa kuna uhusiano wa kiontolojia kati ya jaala ya shujaa, mizimu na jamii. Kutokana na mshikamano huo wa kiontolojia, ng'ombe walitoa maziwa na samli ya kutosha. Watu wakaneemeka na jamii nzima ikastawi. Pia, Rukiza alifungamana na mizimu kupitia vyanzo vyake vya sihiri. Vyanzo vya sihiri vilimwezesha kupata nguvu za kimwili, kiakili na nguvu za sihiri alizozitumia katika mapambano. Aidha, mshikamano wa shujaa na watu wake ulimwezesha kupata taarifa kuhusu vita. Halikadhalika, mshikamano wa shujaa na jamii ulisaidia kutunza siri ya nguvu zake za sihiri mpaka Ruhinda alipotumia uchawi ndipo alipoweza kubaini siri hiyo. Hivyo, shujaa lazima awe na mshikamano na kundi au jumuiya fulani inayomuunga mkono. Mambo haya ni muhimu kwa shujaa na yanaweza kumsaidia asiangushwe (Mulokozi, 1999; 2002). Katika tendi za *Rukiza* na *Mugasha* tumebaini kuwa jaala za mashujaa haziwezi kutimia kama shujaa akijitenga na jamii yake. Hivyo, uhusiano wa kiontolojia kati ya mashujaa na mizimu kupitia tambiko, uganga, sadaka na maombi uliwawezesha kutatua matatizo yao na ya jamii. Halikadhalika, mshikamano wa mashujaa na jamii zao uliwawezesha kushirikiana katika mambo mbalimbali, kama vile uzazi, vita na utatuzi wa changamoto zilizowakabili katika msako wa jaala zao. Kwa upande mwingine, kuvunjika kwa uhusiano wa kiontolojia kati ya shujaa Rukiza na mizimu kumesababisha shujaa kushindwa kutimiza jaala yake ya utawala.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala hii tumebaini kwamba jaala ya shujaa inaundwa na vipengele vya ontolojia ya Kiafrika kama vile kuthamini uzazi, nguvu ya kani, uanthropomofia, kuheshimu wahenga, umoja, mshikamano na ukamilisho wa maumbile na vilivyomo. Kila kipengele cha kiontolojia kimetoa mchango mkubwa katika kuunda jaala za mashujaa wa tendi teule. Mashujaa wametumia uganga na utabiri kutambua na kutatua vikwazo walivyokabiliana navyo katika msako wa jaala zao. Kadhalika, uzazi ni njia iliyotumiwa na mizimu kudhihirisha jaala ya utawala katika tendi. Aidha, kuheshimu wahenga, uanthropomofia na nguvu ya kani ni vipengele vya kiontolojia vilivyowawezesha mashujaa kupata nguvu na ulinzi katika miili yao. Vilevile, vipengele hivyo vimetumika kuimarisha silaha za shujaa kwa kuzipa nguvu za sihiri. Kwa upande mwingine, vipengele vya kiontolojia vimewawezesha mashujaa kupata msaada wa mizimu walipozidiwa na adui. Pia, vipengele vya kiontolojia vimewaunganisha mashujaa na ontolojia ya jamii yao na kuwawezesha kutimiza jaala zao. Kwa upande mwingine uchawi umetumika kuvunja uhusiano wa kiontolojia kati ya shujaa na jamii yake. Hali hiyo imesababisha shujaa kuangukia katika jaala ya kifo badala ya jaala ya utawala. Hivyo, vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vina mchango mkubwa katika kuunda jaala za mashujaa katika tendi za Nanga.

## Marejeleo


Bowra, C.M. (1964). *Heroic Poetry*. London: Macmillan & Co. Ltd.

Carlson, N. R., & Buskist,W. (1997). *Psychology the Science of Behaviour*. London: Allyn and Bacon.

Cobb, N. J. (2001). *The Child Infants, Children and Adolescents*. California: Mayfield Publishing Company.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*.Tasnifu

ya Uzamivu katika fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Deme, M. K. (2009). "Heroism and Supernatural in African Epic Towards a Critical Analaysis". *Journal of Black Studies*, 39,(3), 402- 419.

Deme, M.K. (2009). "The Supernatural in the African Epic Traditions as a Reflection of the Religious Beliefs of African Societies". *Studies in the World Christianity*, 16, (1), 27- 43.

Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa*. Cambridge: Open Book Publishers.

Ilomo, I. F. (2013). *African Religion: A basis for Interfaith Dialogue Today*. Dar es salaam Tanzania: Dar es Salaam University Press.

Innes, G. (1974). *Sunjata Three Mandinka Version*. London: University of London.

Kajosi, S. (2013). *Suala la uzazi katika Ontolojia ya Kibantu na jinsi linavyojitokeza katika Riwaya za Kiswahili.*Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Kagame, A. (1956). *La Philosophie Bantu-Rwandaise de L'Etre*. Bruxelles: Academie Rayoledes Sciences Coloniales.

Kezilahabi, E. (1985*). African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison.

Lord, A. B. (1991). *Epic Singers and Oral Traditions*. London: Cornell University Press.

Lyamuya, H. N. (2014).*Ulinganishi wa Sababu za Kuanguka kwa Shujaa katika Utendi wa Kiswahili na Tendi Nyingine za Kiafrika*.Tasnifu

ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Magesa, L. (1997). *African Religion the Moral Traditions of Abundant Life*. New York: Orbis Books.

Mair, L. (1969). *Witchcraft*. London: World University Library.

Makumba, M. M. (2005). *Introduction to Philosophy*. Nairobi: Paulines Pulications.

Mihanjo, A. (2004). *Falsafa ya Usanifu wa Hoja kutoka Wayunani hadi Watanzania (Waafrika)*. Tanzania: SALVATORIANUM.

Mulokozi, M. M. (1986). *The Nanga Epos of Bahaya: A case Study in African Epic Characteristics*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam:KAUTTU.

Mutembei, A. K. (2000). Fasihi ya Kitaifa na Fasihi ya Kiswahili ni Dhana ile ile? *Mulika*, 26: 9-18. Dar es Salaam: TUKI.

Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. German: Heinemann University.

Mbiti, J. (1991). *Introduction to Africa Religion Second Edition*. Nairobi: East African Educational Publshers L.t.d.

Mbiti, J.S. (2011). *African Religions and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mnenuka. A. (2020). Mizimu katika Ngano za Kiafrika: Uchambuzi wa Ngano Teule, *Mulika*, 39:1-19. Dar es Salaam: TUKI.

Mpalanzi, L. (2019).*Ujitokezaji wa falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethinografia za Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Nkemnkia, M.N. (1999). *African Vitalogy; A step Forward in African Thinking*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Meveli Publishers (MVP).

Tempels, P. (1945). *Bantu Philosophy*. Paris:Presence Africaine.

Ukwamedua, N. U. na Omokpo, V. (2016). “The Ontology of Destiny and Freedom among Igbo-Africans; A Discourse in Existential Metaphysics”. *IDEA*, Xxviii/,(2), 273-286.

Vázques, A.S. (1973). *Art and Society Essays in Marxist Aesthetics*. New York: Monthly Review Press.

Wiredu, K. (2006*). A Companion to African Philosophy*. Malden USA: Blackwell Publishing.